

**SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA PANGANI  
IDARA YA KISWAHILI  
MTIHANI WA KUTANGULIA MWIGO**

**102/2**

**KARATASI YA 2**

(Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya Lugha, Isimu Jamii)

**MACHI, 2013**

**KIDATO CHA 4**

**MUDA: 2 ½.**

**JINA..... NAMBARI.....**

**Jibu maswali yote.**

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

	<b>Swali</b>	<b>Ufleo</b>	<b>Alama</b>
1	Ufahamu.	15	
2	Ufupisho.	15	
3	Matumizi ya Lugha.	40	
4	Isimu Jamii.	10	
<b>JUMLA.</b>		<b>80</b>	

## **1. UFAHAMU – (Alama 15)**

Ustawi wa dola lolote lile wategemea mseto wa nguvu, maarifa chipukizi, uchapuchapu wa barubaru, pamoja na maarifa, upevu, uvumilivu na tajiriba ya wazee. Twaweza kuumithilisha ufanisi wa nchi na jumba la ghorofa lililojengwa juu ya tegemezo: msingi huu ukiwa imara, ghorofa nyingi zaweza kuinuliwa. Nayo imara ye tegemezo hutegemea vyuma imara visivyotetereka na vifaa vinginevyo. Zaidi ya yote haya, mafundi wahusika kama vile wasanifu mjengo, wahandisi, mafundi bomba na wengineo sharti wawe na ujuzi tosha ili kuifanikisha kazi inayohusika; kinyume chake, jengo litaporomoka. Katika taswira hii, twaweza kuelewa ni kwa nini baadhi ya nchi zimestawi huku nyingine zikkitwa ‘ulimwengu wa tatu’. Si kwamba nchi hizi – Kenya ikiwepo, hazitaki kustawi, la hasha. Shida yetu kubwa ni kutozistawisha taaluma zetu ambazo ndizo msingi wa maendeleo, hivyo kuwa na walakini katika utekelezaji. Matokeo? Kulimatia!

Nchi nyingi humu barani mwetu zimekosa kustawi kutokana na kasoro nyinyi tulizo nazo katika uimarishaji wa taaluma zetu. Sababu kuu ni kuwa, wengi wetu hukimbilia kutekeleza kazi mbalimbali hata bila ujuzi wowote katika taaluma inayohusika. Sisi husema ‘kazi ni kazi’ na mradi ‘unaangukia’ kazi yoyote, unaifanya bila kujali yafaa kufanya vipi. Na kama hujui yafaa kufanya kwa namna gani utaifamya vipi? Hali hii ya kufanya ‘kazi yoyote ipatikanayo’ hutokana na ukweli kuwa sisi hatujali kama tuna vipawa vya kufanya kazi fulani. Wala suala la kipawa haliliwi nguvu inayostahili humu mwetu. Si ajabu kuona kijana aliye na kipawa fulani akikosa kukivuvia kwa kuwa labda hata hatambui kuwa anacho. Wengine pia huvunjwa moyo na watu waliowazingira kwa kuwaambia kuwa vipawa hivyo havifai. Hata wazazi huchangia katika hili. Kwa mfano mtoto aliye na kipawa cha uigizaji, uchoraji, uchongaji, uimbaji, ni rahisi kuvunjwa moyo na wavyele wake kwa kuwa eti kazi zinazoandamana na vipawa hivi sio za hadhi; au zingine kama uanamuziki na uigizaji kuchukuliwa kama zisizo na mbeko, eti zina ukora. Je, ni kweli?

Wengi wa wakembe wetu hukosa kuvitambua vipawa vyao, hivyo kukosa kuendeleza utaalamu unaohusiana navyo kwa kukosekana kwa *mtalaa* wa kuvichochea katika mfumo wetu wa elimu. Kwa sasa, mfumo wetu aghalabu unasisitiza kupita na kwenda chuoni. Si vibaya, lakini pamoja na hili, wafaa kuvitambua na kuvikuza vipawa walivyo navyo vijana ili wavitunge kitaaluma katika siku za halafu. Vitambuliwe mapema shulenii ila sio vyuoni. Kunao wanagenzi wengine pia ambaao, licha ya kuvitambua vipawa vyao, hawavifukutii kamwe, huvipuza na kujisukuma katika taaluma ambazo hazikuwafaa kamwe. Kunao wengine ambaao hutamani na kuingilia taaluma fulani fulani, si kwa kuwa wanazipenda, bali kwa kuwa wandani wao wanazishiriki. Hawajui kuwa *kibaya chako si kizuri cha mwenzio*. Huliona tanga la nguo wakalisahau la miyaa. Msukumo huu huwafanya hata kujitumbukiza katika taaluma wasizoweza kumudu, hivyo kushindwa kusukuma nyenzo za maendeleo ya nchi.

Kuna wengine ambaao huziandama taaluma sio kwa kupenda kwao, bali kwa kushurutishwa na wazazi, watu wa mlango wao ua wadhamini wao. Wengi huwachagulia eti kwa kuwa ukoo wao ni wa taaluma fulani, huku wengine wakiiangalia hadhi ya kazi inayohusika. Nao vijana hukosa ukakamavu wa kujiamulia na kukubali shingo upanda. Hata hivyo, kunao wajitosao bila kushurutishwa ili eti wapate hadhi. Matokeo huwa kwamba kijana huzifanya kazi hizo *chati wala si kwa dhati*.

Wengine ‘huipenyeza’ kwenye taaluma fulani eti kwa kuwa wamekosa nyingine. Si ajabu basi kutokana na ukosefu wa ajira kumwona mtaalamu wa mifugo eti akiwa mwalimu, mwalimu akiwa dereva, tabibu akiwa mkulima hali zaraa haimudu. Matokeo ya haya ni kuifanya kazi kiholela na kuichanganya kama biwi la takataka. Pamoja na

hawa, kunao waingiao katika taaluma fulani kwa kuwa huko kuna malipo chungu nzima. Hawa ni waongozwao na matumbo yaliyosheheni uroho. Sikatai kuwa hata mie ningependa malipo bora, ila tuongozwapo na pato, pindi tupatapo palipo na malipo bora zaidi au tusiporidhishwa na tunachopata katika hali hii ngumu ya maisha, mara tutajing'atua kazini na kuacha miradi iliyotekelezwa nusu nusu.

Na labda heri kujing'atua kuliko kuaminiwa usilotekeleza. Maadamu wengi hawako kazini wanazofanya kwa kuwa wanazipenda, si ajabu kuwakuta maafisa wakipiga zohali au hata kukaa tutwe ofisini. Wengine waweza kuwaita mabosi wa chai, kwani hupatikana ofisini majira ya chai pekee. Wengine huketi kutwa wakidurusu magazeti, hali kunao wayaning'izayo makoti vitini na kuyoyoma. Hiki ni kilele cha *ukunguni, uzandiki* na usaliti kwa nchi. Matokeo yake ni maafa kwa iktisadi ya bara letu – yadorora kila uchao.

Ili kupata suluhu katika jambo hili, sharti kila mmoja wetu ashiriki katika kuitambua, kuikuza kuikomaza, kuiendeleza, na kuitumia taaluma ya kila kijana au hata mtoto. Twaweza kuuiga mfano wa Wazungu wafanyavyo kwao. Wao hujitahidi kuvitambua vipawa vya wanao wangali wachanga, hali ambayo huwasaidia ~~ku~~ kuzikuza taaluma zao tangu hapo. Si ajabu kukutana na mtoto wa miaka kumi ajuaye kwa yakini tayari atafanya kazi gani atakapokomaa. Naye kijana akishajua atakachofanya, afaa kufanya utafiti ili kufikia kina cha taaluma yake. Afaa kutafuta ~~maoni~~ ya wengine, wazee kwa vijana na awe tayari kukosolewa na kuelekezwa ili kufikia kilele cha ujuzi na ndipo aipende taaluma yake zaidi. Wazazi na walimu wana jukumu la kuelekeza, kusaidia katika ukuaji na kuwapa nafasi wanagenzi wanaovikuza vipawa vyao.

Walimu pia wanafaa kuchochea na kutoa changa moto kwa wizara ya elimu ili nayo ikuze *mtaala* ambaa utawafaa wanafunzi katika uenezaji wa vipawa, hivyo kuendeleza taaluma za wanafunzi. Ileweke hapa kuwa, sio kwamba mtaala wetu umepungukiwa sana – ngaa unayakuza maarifa ya elimu kijumla. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa unaendeleza elimu kinadharia tu, sio *elimu tekelezi*. Hili lafaa kuangaliwa, kwani huwacha wanafunzi wakielea, hawavitambui vipawa vyao, hivyo kuvitambua uzeeni. Wazungu husema kuwa mbwa mzee hafunzwi kuwinda. Nasi mbona tusiwafunze watoto wetu taaluma ziwa lazo wangali chipukizi? Sharti tuzibadili sera zetu. Mwisho, tufahamu kuwa taaluma hukua kama mti. Jinsi mti uanzavyo kutoka kwa mbegu, ukawa mche, ukapandwa, labda *ukapandikizwa*, ukapaliliwa, *ukapogolewa*, huku waendelea kunyonyiziwa maji na hata dawa inapohitajika, bila kusahau kuwa unalindwa dhidi ya maadui wowote wale, ndivyo ilivyo na taaluma. Hali hizi zahitaji muda mwingu na uvumilivu mwingu. Nao mwangaza hupatikana baada ya saa nyingi za kiza totoro.

#### Maswali:

- 1) Nakili kichwa mwafaka cha kifungu hiki. (al 1)

.....  
.....

- 2) Je, ustawi wa dola hutegemea vitu gani kulingana na yaliyomo kwenye kifungu hiki? (al 2)

.....  
.....  
.....

- 3) Ni nini kinachofanya nchi hasa za ulimwengu wa tatu kubaki nyuma kimaendeleo?  
Taja sababu tano kutokana na kifungu. (al 5)

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

- 4) Vijana hupotoka vipi kuhusiana na vipawa vyao? (al 2)

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

- 5) Mwandishi anamaanisha nini anaposema ‘huliona tanga la nguo wakalisahau la miyaa’? (al 1)

.....  
.....  
.....  
.....

- 6) Eleza maana ya methali ‘kibaya chako si kizuri cha mwenzio,’ kama ilivyotumika kwenye kifungu. (al 2)

.....  
.....  
.....  
.....  
.....

7) Ni nini maana ya maneno yafuatayo kulingana na kifungu? (al 2)

(i) Piga zohali -

(ii) Kwa chati wala si kwa dhati -

## 2. **MUHTASARI**

"Heshima si utumwa," ni usemi unaomaanisha ya kwamba heshima si jambo linalodunisha au kudhalilisha hadhi ya mtu. Kwa hakika, mtu anapomheshimu mwenzake huwa pia anajiheshimu yeye mwenyewe. Jambo hili humwezesha binadamu kuishi kiutu.

Katika tamaduni zetu watu hufunzwa kuwaheshimu wakubwa wao tangu utonni. Jambo hili husisitizwa kwa mapana na mrefu yake. Mtoto anayedhihirisha utovu wa heshima husutwa, akakemewa na kukashifiwa. Wazazi wake nao hutwa lawamani kwa kutotimiza wajibu wao. Hata fasihi simulizi ya kiafrika kama vile ngano, nyimbo na methali hujihusisha na maudhui ya heshima.

Ingawa nidhamu ni jambo linalositisizwa sana, inashangaza kuwa vijana wengi hawalishughulikii kwa dhati. Kila uchao tunalazimika kushika tama huku tukijiuliza maswali mengi kuhusu utovu huu wa adabu. Je, ni wazazi ambao wameuweka pembezoni wajibu wao, ni walimu wasiotekeleza vilivyo jukumu lao? Tungeweza kusema kuwa haya ni matokeo ya taashira za utamaduni wa kigeni kuititia vyombo mathalani televisheni, cinema, video na vitabu? Hiki ndicho kitendawili ambacho kinatuzidi nguvu.

Jambo muhimu limpasalo mtu yeyote kulizingatia daima, kama tunavyoendelea kufafanua ni heshima. Tunafahamu kwamba hata wanyama huwaheshimu wazazi wao ijapokuwa wanapokomaa hushindwa kuwapambanua. Hata hivyo wakati wakiwa wadogo hawana uwezo wa kuyakabili mazingira makali bila msaada, huwaheshimu wazazi wao. Basi ikiwa wanyama wanawaheshimu wazazi wao seuze binadamu aliyetunukiwa akili nyingi na muumba wake? Heshima kwa wazazi si mdomo tu bali pia ni vitendo.

Mtu hulelewa na wazazi wake mpaka akaanza kujitegemea mwenyewe. Lakini hata anapokuwa mtu mzima, wazazi wake bado humchukulia kuwa mtoto. Wazazi wake waanzapo kuzeeka, yeye hutarajiwa kuwashika mkono. Ni wakati huu ambapo majirani humweka kwenye mizani kupima ubinadamu wake. Hapo ndipo utu wake unapobainika.

Ni jukumu la watoto kuwasaidia wazazi wao. Misaada yao itolewe kwa dhati na kwa moyo. Si jambo la heshima mtu kuenda kwa wazazi wake baada ya kukaa mbali nao kwa muda mrefu, na katika kuwapa zawadi alizoteua awaambie, "Nimewaletea zawadi hizi kwani najua kwa vyovoyote hamdiriki kuzipata. Najua wazi kwamba hamna ujuzi, maarifa, mbinu na akili kama zangu." Hiyo ni dharau kubwa sana.

Wakati mtu anapotangamana na wazazi wake lazima awaonyeshe ukarimu na moyo wa kupenda. Akipata uwezo wa kuwatunukia zawadi au kitu chochote kingine, jambo liwezalo kuwaudhi zaidi ya yote, asiwalize wazazi wake watakapokoma kutegemea msaada wake. Aidha asiwatajje muda ambao amekuwa akiwasaidia kwa sababu wataudhika sana. Ni muhimu kukumbuka kwamba mtu hawezi kulipa gharama ya malezi yake.

**Maswali.**

- a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa taarifa, fupisha aya sita za kwanza. (Maneno 70 – 80). (al 8, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

- b)** Kwa kuzingatia aya mbili za mwisho, eleza mapendekezo ya mwandishi kuhusu mtu kuwasaidia wazazi wake. (Maneno kati ya 35 – 45.) (al 5, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

### **3. MATUMIZI YA LUGHA – (Alama 40)**

**1) Eleza sifa mbili za sauti /ng'/** (al 2)

(i)

(ii)

**2) Tumia kirejeshi ngeli katika sentensi.**

Mtoto ameangusha kuta.

(al 1)

**3) Kamilisha sentensi ukitumia –o-ote.**

(i) Shimoni, panya hazunguki \_\_\_\_\_

(ii) Bizari \_\_\_\_\_ hufaa kwa matumizi.

**4) Geuza sentensi katika hali ya kuamuru.**

(i) Nyinyi mfanye kazi

.....

(ii) Tafadhali msameheane.

.....

**5) Huku ukitoa mfano, fafanua dhana ya vitenzi sambamba.**

(al 2)

**6) Tunga sentensi yenye kiima na kiarifa.**

(al 2)

**7)** Nyambua kitenzi la katika kauli ya kutendesheana kisha utumie mnyambuliko huo katika sentensi. (al 2)

**8)** Andika ukubwa wa wingi wa sentensi ifuatayo:  
Kilichomsononesha panya ni neti iliyotengeneza uzio. (al 2)

**9)** Huku ukitoa mfano, eleza dhana ya kauli ya kutendata. (al 2)

**10)** Tunga sentensi yenyewe muundo ufuatao:  
KN (W + S) + KT (T + KE : E + E) (al 2)

**11)** Huku ukitoa mfano wa sentensi eleza maana ya shamirisho kitondo. (al 2)

**12)** Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari.

Kumbe huyu ni askari jela?

(al 3)

**13)** Geuza nomino zifuatazo ziwe vitenzi.

(al 2)

Taarifa .....

Matumizi .....

**14)** Tambua aina za vishazi katika sentensi ifuatayo.

(al 2)

Nitakuona kesho jioni endapo nitakuja mijini.

**15)** Akifisha.

(al 2)

Nilimuuliza Jane je wewe utaweza kazi hii kweli

**16)** Tunga sentensi moja yenyе vitenzi halisi viwili.

(al 2)

**17)** Eleza maana ya kimbo.

(al 2)

**18)** Andika katika msemo wa taarifa.

(al 4)

“Sasa tumemsubiri mama, kwa muda mrefu. Asipowasili tutaenda zetu kesho asubuhi,” Amina alisema.

**19)** Tunga sentensi moja yenyé nomino ya kitenzi – jina na nomino ya wingi. (al 2)

#### **4. ISIMU JAMII – (Alama 10)**

Kwa kurejelea hoja zozote tano eleza sifa za sajili katika muktadha wa mazungumzo kati ya wataalamu.